

**HOTUBA YA MHE. ANGELLAH JASMINE KAIRUKI (MB.) WAZIRI WA NCHI,
OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA)
KWENYE UZINDUZI WA BODI YA KIMA CHA CHINI CHA MSHAHARA KATIKA
SEKTA YA UMMA, UKUMBI WA MIKUTANO WA OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI
YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA), DAR ES SALAAM
TAREHE 29 APRILI, 2017**

- *Dkt Laurean Ndumbaro, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora);*
- *Ndugu Getrude K. Mpaka, Mwenyekiti wa Bodi ya Kima cha Chini cha Mshahara katika Sekta ya Umma;*
- *Ndugu Wajumbe wa Bodi;*
- *Ndugu Waandishi wa Habari;*
- *Mabibi na Mabwana;*

Habari ya Asubuhi,

Kwanza kabisa, napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima na afya njema hata tukaweza kukutana leo kwa ajili ya uzinduzi wa Bodi yetu ya Kima cha chini cha Mshahara kwa Sekta ya Umma.

Pia, napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Wajumbe wote kwa kukubali wito wangu wa kuhudhuria siku hii muhimu ambao nimeutoa katika kipindi kifupi sana.

Nipende pia kuwashukuru Viongozi na Watendaji wa Ofisi ya Rais, (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) kwa Maandalizi mazuri mliyoyafanya kufanikisha shughuli hii muhimu.

Ndugu Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi;

kabla ya kuendelea na hotuba yangu napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuteuliwa na kukubali uteuzi wangu kuwa mwenyekiti wa kwanza wa Bodi hii. Ni matumaini yangu na sina shaka kwamba kwa maarifa, ujuzi na uzoefu ulionao, utalibeba jukumu hili la kuongoza Bodi hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kama ilivyokusudiwa.

Pia, napenda kuwapongeza Wajumbe wote kwa kukubali uteuzi wangu na hivyo kuwa wajumbe wa Bodi ya Kwanza ya Kima cha Chini Katika Sekta ya Umma tangu

